

## Kwa nini watoto wengine wanahitaji kufanyiwa ukaguzi mwingi wa uwezo wa kusikia ikiwa wameshafaulu ukaguzi wa baada ya kuzaliwa?

Upungufu wa uwezo wa kusikia unaweza kutokea wakati wowote. Ingawa kufaulu ukaguzi wa baada ya kuzaliwa ni mwanzo mzuri, watoto wengine wana vipengele hatari vinavyohusiana na matatizo ya kusikia yanayoweza kutokea baadaye maishani.

Hizi ni baadhi ya sababu kwa nini kufuatilia uwezo wa mtoto kusikia katika maisha ya utotoni kunapendekezwa:

- kuchelewa kunena na/au ufahamu wa lugha
- historia ya familia ya upungufu wa uwezo wa kusikia kabisa utotoni
- tofauti zinazoonekana kichwani, usoni, shingoni au masikioni
- dawa fulani zinazopewa mtoto baada ya kuzaliwa
- dalili zinazohusiana na upungufu uwezo wa kusikia
- kulazwa kwenye kitengo cha wagonjwa mahututi cha watoto wachanga
- kuzaliwa kabla ya wakati wake (chini ya wiki 37)

Mzazi au mhudumu mwenye wasiwasi ndiyo sababu moja muhimu kabisa ya mtoto kufanyiwa ukaguzi wa kusikia.

VTEHDI itakutumia wewe barua na daktari wa kwanza wa mtoto wako ikiwa ukaguzi wa kufuatilia unapendekezwa.

## Programu ya Ugunduzi na Matibabu ya Matatizo ya Kusikia Mapema ya Jimbo la Vermont ni nini?

Programu ya Ugunduzi na Matibabu ya Matatizo ya Kusikia Mapema ya Jimbo la Vermont (VTEHDI) hutoa usaidizi, mafunzo, na huduma za usimamizi kwa familia na watoto wao, na kwa wahuduma wa jamii. Ubia huu husaidia kwa kutoa rufaa mapema kwa upimaji wa uchunguzi na huduma za matibabu ya mapema.

Tunazipa familia na watoa huduma mapendekezo ya ufuatiliaji kwa huduma endelevu ya kusikia kulingana na hatari na mahitaji ya mtoto.

Programu yetu hushirikiana na wakala na mashirika ya jimbo na kitaifa kutimiza malengo ya 1-3-6 ya ugunduzi na matibabu ya matatizo ya kusikia mapema.

### Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi:

**Simu:** 1-800-537-0076 au 1-802-651-1872
**Barua pepe:** VTEHDI@vermont.gov
**Tembelea:** www.healthvermont.gov/family/hearing

Kijitabu hiki kinapatikana kwa lugha zingine kwenye tovuti yetu: www.healthvermont.gov/family/hearing/resources

VERMONT
**Idara ya Afya**

Ugunduzi na Matibabu ya Matatizo ya Kusikia Mapema ya Jimbo la Vermont
Idara ya Afya ya Mama na Mtoto
108 Cherry Street S.L.P. 70
Burlington, Vermont 05402
www.Healthvermont.org

# *Mtoto wangu anaweza kusikia?*



Maelezo kwa familia kuhusu

## UKAGUZI WA UWEZO WA KUSIKIA KWA WATOTO WACHANGA NA ZAIDI

**Idara ya Afya ya Vermont**
**Ugunduzi na Matibabu ya Matatizo ya Kusikia Mapema ya Jimbo la Vermont**
**Idara ya Afya ya Mama na Mtoto**

## Kwa nini watoto WOTE wachanga wanafaa kufanyiwa ukaguzi wa uwezo wa kusikia baada ya kuzaliwa?

Watoto huanza kupata uwezo wa kunena na lugha kuanzia wakati wa kuzaliwa. Mwaka wa kwanza wa mtoto ni muhimu kwa kukua kwa uwezo wa kunena na lugha wa kawaida. Wakati sauti haziwezi kusikika, ukuaji wa lugha unachelewa. Upotevu wa uwezo wa kusikia unaweza kukosa kutambuliwa kwa urahisi katika miaka ya mapema maishani. Wazazi wengi wanafikiria wanaweza kujua kama mtoto hawezi kusikia. Lakini huwa sio hivyo wakati wote.

Takriban watoto watatu wachanga kati ya kila watoto 1,000 wana upungufu fulani wa uwezo wa kusikia. Ni nusu ya watoto wanaochunguzwa kwa matatizo ya kusikia peke yake ndiyo wana historia inayojulikana ya matatizo ya kusikia katika familia zao au vipengele vingine vya hatari ya upungufu wa uwezo wa kusikia. Ukaguzi wa kusikia wa watoto wachanga unaweza kugundua uwezekano wa kupoteza uwezo wa kusikia katika siku chache za kwanza za maisha.

## Mtoto wangu atafanyiwa ukaguzi wa uwezo wa kusikia lini?

Mtoto wako anafaa kufanyiwa ukaguzi wa uwezo wa kusikia kabla ya nyinyo kuondoka hospitalini. Hospitali nyingi zitakagua uwezo wa mtoto kusikia baada ya umri wa saa 12-24.

Ikiwa ulijifungua nyumbani, mkunga wako atamkagua mtoto wako ndani ya wiki ya kwanza ya maisha yake.



## Ni nani atakagua uwezo wa kusikia wa mtoto wangu?

Ukaguzi wa uwezo wa kusikia unaweza kufanywa na daktari wa masikio, wauguzi, wataalamu wenye mafunzo, wataalamu wa kupumua, au wakunga.

## Uwezo wa kusikia wa mtoto wangu utafanywa vipi?

Aina mbili za ukaguzi wa uwezo wa kusikia ni Jibu la Shina Gongo la Ukaguzi Otomatiki (AABR) na Utoaji wa Otoakoustiki (OAE). Mtoto wako anaweza kukaguliwa na mbinu moja kati ya hizi au mbinu zote mbili.

Ukaguzi ni salama, haraka, na bila maumivu. Watoto wengi huwa wamelala wakati wote wa ukaguzi na matokeo yanapatikana wakati ukaguzi unakamilika.

## Kuna uwezekano wa matokeo gani ya ukaguzi wa uwezo wa kusikia wa mtoto wangu mchanga?

**FAULU** inamaanisha hakuna hatua zaidi inahitajika kwa wakati huu.

**RUFAA** inamaanisha mtoto wako hakufaulu ukaguzi wa uwezo wa kusikia katika sikio moja au masikio yote mawili. Hii haithibitishi upungufu wa uwezo wa kusikia, lakini ukaguzi wa uwezo wa kusikia unahitaji kurudiwa.

**Ukaguzi haukukamilika au Ulijaribiwa; Hakuna Matokeo Yanayopatikana** inaonyesha kwamba ukaguzi umesimamishwa kabla ya kukamilika na ukaguzi mwingine unahitajika. Jambo hili hutokea kwa sababu ya kiwango cha shughuli cha mtoto au matatizo ya kifaa chenyewe.

Matokeo ya ukaguzi wa uwezo wa kusikia wa mtoto wako yatashirikishwa kwa daktari wa kwanza wa mtoto wako na sisi, Programu ya Ugunduzi na Matibabu ya Matatizo ya Kusikia Mapema ya Jimbo la Vermont (VTEHDI).

## Na ikiwa mtoto wangu hakufanyiwa ukaguzi wa uwezo wa kusikia au anahitaji ukaguzi mwingine?

Programu ya VTEHDI itawasiliana na wewe. Wafanyakazi wetu watakusaidia kuamua utakapowekesha maidi ya ukaguzi kama mgonjwa wa nje.

Ukaguzi wa uwezo wa kusikia unapatikana katika :

- hospitali za jamii
- kliniki zingine za matibabu ya kusikia
- kliniki zingine za matibabu ya watoto.



## Malengo ya 1-3-6 ya Kitaifa na Jimbo

Viwango vya huduma vya kitaifa na malengo ya VTEHDI ni kukagua uwezo wa kusikia wa watoto wote wachanga kabla ya kuondoka hospitalini au wanapofikisha umri wa **mwezi 1**. Ikiwa mtoto wako hatafaulu mchakato wa ukaguzi wa kwanza, basi ukuaguzi zaidi unahitajika. Watoto wenye kiwango chochote cha upungufu wa kusikia watakuwa na fursa bora ya ukuaji wa kawaida wa kunena na lugha ikiwa watachunguzwa wanapofikisha umri wa **miezi 3** na kuandikishwa katika huduma za usaidizi wanapofikisha umri wa **miezi 6**.